# JARIBIO LA MTIHANI STEP FLYER

## DARASA LA NANE - MWAKA 2023

## KISWAHILI:LUGHA

STEP FLYER (002) (8)

***Muda:Saa 1 Dak 40***

***SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI***

1. Umepewa kijikaratasi hiki cha maswali na karatasi ya majibu. Kijikaratasi hiki kina maswali 50.
2. Katika karatasi ya majibu hakikisha umeandika:-
   *(i) Jina lako* *(ii) Jina la shule yako* *iii). Nambari ya KNEC*

**Soma vifungu vifuatavyo kisha ujaze nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua jibu lifaalo zaidi.**

Ufisadi ni ___1___. Mtu anayejihusisha na ufisadi huitwa ___2___. Ndiposa atapigiwa msemo, fulani ali___3___. Baa hili la shida ___4___ kuangamiza___5___ nyingi hapa duniani ___6___ maafa mengi duniani. Ni wazi kuwa asilimia yetu kubwa ___7___ nao kwa njia moja ua nyingine. Ni lazima kama ___8___ tushirikiane kwa ___9___ kumaliza nduli huyu ili ___10___

1. A. kumpa mtu asichostahili
   B. kupewa kitu asichostahili
   C. Uharibifu wa mali ya umma
   D. kupewa pesa za nchi

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2. | A. ufisadi | B. mfisadi | C. fisidi | D. wafisadi |
| 3. | A. kula kalenda | B. zunguka mbuyu | C. kula mwande | D. kunywa chai |
| 4. | A. inayotisha | B. linalotutishia | C. linaloutishia | D. inayotishia |
| 5. | A. jamaa | B. mataifa | C. jamii | D. watu |
| 6. | A. lenye | B. yenye | C. zenye | D. chenye |
| 7. | A. tumejihusisha | B. imejihusisha | C. zimejihusisha | D. wamejuhusisha |
| 8. | A. sheria | B. mauti | C. ibada | D. afya |
| 9. | A. ujino na ukucha | B. hamu na ghamu | C. raghba ya mkanja | D. guu mosi guu pili |

10. A. tugonge gogo tusikie mlio wake
    B. tukate ubeleko kabla ya mwana kuzaliwa
    C. tuivute ngozi kwetu
    D. tukiwahi chuma kingali moto

Ali alikuwa na ___11___ kubwa ya masomo. Kiu ___12___ masomoni kilikuwa sawa na hamu na ghamu na mama kupata mwana. Walimu nao ___13___ kumsaidia. Ali alijua na pia ___14___ mwalimu mkuu angemtafutia ___15___ amlipie karo ya masomo yake kwani kwao walikuwa maskini sana.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11. | A. ari | B. hali | C. tayari | D. chuku |
| 12. | A. chake | B. yake | C. lake | D. zake |
| 13. | A. walimtolea | B. walijitoa | C. walijitolea | D. walimtolea |
| 14. | A. kuangalia | B. kuamua | C. kutazama | D. kutazamia |
| 15. | A. mthamini | B. mdhamini | C. mhadhiri | D. mfawidhi |

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu sahihi***

16. ***Tambua aina tofauti za ki***
Ukirusha kipira hiki kitapotea.
A. Kitendo, chombo wakazi
B. Mtendaji, umoja, kiashiria
C. Nafsi, udongo, kitenzi
D. Masharti, udongo, kiambishi ngeli

17. **Ni nomino gani dhahania?**
A. Boresha
B. Usahaulifu
C: Wenzo
D. Jukwaa

18. Ni methali gani inayolingana na maelezo haya. Ni bora kuwa na ndugu mbaya anayekusaidia wakati wa shida kuliko yule wa mbali asiyekusaidia
A. Mui huwa mwema
B. Damu ni nzito kuliko maji
C. Ndugu mui heri kuwa naye
D. Mchumia janga hula na wa kwao

19. Uwiano wa sauti katikati na mwisho wa mshororo ni __________.
A. mloto B. mizani
C. kina D. kibwagizo

20. Mshenga kwa posa ni kama _______ kwa maji.
A. mzegamzega B. topasi
C. kungwi D. bawabu


21. Chagua sentensi iliyotumia **ka** kuonyesha mfululizo
A. Mwelekeze mzee akate chakula
B. Mpira uligongwa ukadunda ukagonga kioo na kukipasua
C. Kiti hicho kidogo kimeundika vizuri
D. Tawi la mti lilianguka kacha lilipovunjika

22. Maradhi mengi yameweza kuthibitiwa.
Neno mengi limetumika kama _______
A. kivumishi kimilikishi
B. kivumishi cha sifa
C. kivumishi cha pekee
D. kivumishi cha idadi

23. ***Andika kinyume cha***
Fahali mpole ametoka nje
A. Ng'ombe mkali ameingia ndani
B. Maksai mkali ametoka nje
C. Fahali mkali ametoka nje
D. Bakari mkali ameingia ndani

24. Chura ni mnyama mdogo aendaye kwa kuvuka. Chura pia ni _____________
A. Anayefanya kazi ya kufunga mizigo chomboni
B. Anayetumwa kupeleka ujumbe wa posa
C. Anayetunza na kufunza farasi
D. Anyeibuka wa mwisho katika mchezo wa watoto

25. ***Taja umbo hili.***



A. mchinjo kali
B. hiram
C. tufe
D. mche

26. _____________ ni kiungo ambacho husaga chakula katika mwili wa ndege.
A. Firigisi
B. Kongosho
C. Nso
D. Wengu

27. **Chagua sentensi inayoonyesha istiara**
A. Mlo tulioula ulikuwa mtamu kama hahoe
B. Mwizi alikamatwa na kubebwa hobelahobela
C. Alimwangalia shashimamishi bila ya kunionea huruma
D. Maswali yote yalikuwa mboga tu

28. ***Andika kwa umoja***
Nyenzo madhubuti hutumiwa kuinulia majabali
A. Nyenzo dhubuti hutumiwa kuinulia jabali
B. Uwezo madhubuti hutumiwa kuinulia jabali
C. Wenzo mathubuti hutumiwa kuinulia jabali
D. Uwenzo dhubuti hutumiwa kuinulia majabali

29. **Mwana wa punda huitwa __________**
A. kihongwe
B. kiwavi
C. kivinimbi
D. kipunda

30. Shungi ni kwa nywele kama vile bumba ni kwa
A. pesa
B. nguo
C. pamba
D. nyuki

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31-40.**

Anda alikuwa kijana yatima. Wazazi wake waliuaga ulimwengu yeye akiwa mkembe. Jambo lililompa moyo kijana huyu ni ahadi ya mjombawe kuwa angemlea vyema.

Wahenga walitueleza kuwa ahadi ni deni lakini Sango mjombake Anda hakuweka ahadi yake. Alipomchukua Anda alimpa kila aina ya mateso. Sango alimwambia mkewe kuwa hakukuwa na haja ya kumlisha mtoto asiyefanya kazi yoyote. Hatimaye alikataa kumlipia karo ya shule, jambo lililomfanya aache kusoma. Aliachia darasa la tano.

Kumtoa Anda shuleni hakukotosha, yeye na mkewe walimpa kazi ya sulubu nyumbani. Kila asubuhi alishurutishwa kufua mtumba wa nguo, kuosha vyombo na kupiga deki. Isitoshe Sango na mkewe walimpiga na kumtupia vipande vya matusi. Mtoto wa pekee wa Bwana Sango aliitwa Koto. Alikuwa akisoma shule ya Bweni jijini. Shule zilipofungwa alirudi nyumbani akiwa na huzuni kubwa. Sababu ya kujawa na biwi la simanzi ni kuwa alikuwa mkia katika somo la Hesabu na Kiswahili. Wazazi wake walimkaripia. Kwa nini ushindwe na watoto wengine shuleni?" Babake alimkemea.

Anda alihuzunishwa na hali hiyo. Jioni yake alimwambia Koto kuwa angemsaidia kudurusu. Anda alikuwa mwerevu na shuleni alikuwa akiongoza tangu darasa la kwanza. Kila siku walijifungia chumbani na kumfunza Koto hadi likizo ikaisha. Mwalimu wa Koto aliona maajabu. Koto alikuwa sasa anafunza wengine Hesabu na Kiswahili. Mwalimu alitaka kujua kilichomsababisha awe mwerevu hivyo. Kofu alimweleza juu ya Anda. Kisha alimweleza kuwa yeye hasomi tena. Mwalimu alimpelekea habari Mwalimu Mkuu ambaye alitaka kumwona Anda.

Mwalimu Mkuu alipelekwa nyumbani na Koto. Walipofika tu Sango alikataa kufungua lango. Mwalimu aliwaeleza polisi ambao walifika haraka. Anda aliokolewa kutoka katika mateso hayo. Mwalimu mkuu alimpa nafasi ya kusoma shuleni kwake. Sango na mkewe wakawa na mashtaka ya kujibu.

**31.** Anda hakujua kwamba __________
A. Sango aliweka ahadi
B. Sango ni mjombake
C. Angepata shida maishani
D. Angesoma vizuri

**32.** Maneno **'akiwa mkembe'** yana maana akiwa
A. mdogo
B. mchanga
C. kubwa
D. mnyonge

**33.** Methali ***'ahadi ni deni'*** inatufunza kuwa
A. tunapoahidiwa tusifanye mzaha
B. tukiombwa pesa tutoe
C. tukiahidi mambo tutimize
D. tusikubali kudai madeni

**34.** Kwa nini Sango na mkewe walimtesa Anda?
A. Walikuwa na wivu
B. Walikuwa hawana mtoto
C. Walikuwa wazee
D. Walikuwa katili

**35.** Neno **'kushurutishwa'** ni sawa na
A. alipigwa
B. alilazimishwa
C. aliagizwa
D. aliombwa

**36.** Ni kauli ipi si ya kweli __________
A. Anda alikuwa mwerevu
B. Sango hakumpenda Anda
C. Mwalimu wa Koto alimwokoa Anda
D. Sango alikuwa na watoto wengine

**37.** Kulingana na taarifa, maana ya **alimkemea** ni
A. alimwonya
B. alimgombeza
C. alimwita
D. alimtukuna

**38.** Kulingana na kifungu, methali ipi inalenga maisha ya Anda?
A. Fimbo ya mbali haiuwi nyoka
B. Mola hamtupi mja wake
C. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu
D. Mla ni mla leo, mla jana kalani

**39.** Ni hatia gani walifanya wazazi wa Koto?
A. Kumfanya Anda afue
B. Kumdharau Anda
C. Kumkemea mwanawe
D. Kumnyima Anda haki yake

**40.** Kichwa kinachofaa zaidi kisa hiki ni?
A. Sango na mkewe
B. Tutimize ahadi
C. Koto shuleni
D. Mwalimu mkuu wa Koto

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu swali 41-50.***

Ni ukweli usiopingika kuwa hali ya mawasiliano ya siku hizi imeboreshwa na kurahisishwa sana. Sio siku za kisogoni ambapo watu wengi waliwasiliana japo kwa taabu nyingi.

Kuanzia siku za mababu zetu, hadi miaka ya hivi majuzi, watu wengi hawakuwa na vifaa vya mawasiliano ambavyo siku hizi vimepatakaa kila mahali. Ilikuwa vigumu sana kumpata mtu na simutamba labda wale mabwenyenye tu, yaani wale watu na vyao. Redio nazo hazikupatikana kila mahali kama siku hizi. Labda ungepata redio moja ikisikizwa na watu katika kijiji kizima. Runinga nayo hata usiseme.

Ile huduma iliyotolewa na Shirika la Posta na simu hapa nchini iliwaokoa wengi katika kutuma na kupokea barua. Aidha, shirika hili liliwafaa sana watu enzi hizo kwani mja angetaka kutuma ujumbe wa dharura, angetuma telegramu na ingepokelewa upande wa pili baada ya muda mfupi labda siku moja au mbili hivi. Njia hii ilionekana kama ya haraka ya kutuma ujumbe kwani barua nyakati hizo zingechukua hata wiki tatu ama mwezi mmoja kumfikia aliyenuiwa.

Hata hivyo kutokana na uvumbuzi wa teknolojia mpya mambo yalibadilika kabisa. Uvumbuzi wa tarakilishi na mitambo mingine ya teknolojia ukabadilisha kabisa sura ya mawasiliano. Kiza kilichomfunika macho mwanadamu kikaondolewa na mwanga wa teknolojia mpya. Siku hizi si ajabu kumwona hata watoto wakiwa na simu za mkono, tarakilishi za kupakata na kadhalika. Mitambo ya mawasiliano imezagaa kote. Ukitaka kusema na aliye ulaya unabonyeza tu kiduda kwenye tarakilishi yako naye anapata habari papo hapo! Maajabu yalioje!

Kwa kutumia hizo simu za mkononi, mtu anaweza kutuma ujumbe mfupi ikiwa hataki kumpigia simu anayewasiliana naye. Kwenye tarakilishi, pia waweza kutuma baruameme au barua pepe. Aidha kuna kipepesi ambacho ni kifaa kinachotumika kuitumia au kupokea ujumbe wa barua kieletroniki. Teleksi nayo ni njia ya mawasiliano ya simu ambayo husafirisha ujumbe ulioandikwa kama ulivyo. Uzuri wa njia hizi zote za mawasiliano ya kisasa ni kuwa, ujumbe unapotumwa mtu huupata papo hapo.

**41.** Chagua jibu sahihi linalotoa maelezo sahihi ya neno mawasiliano
A. upashanaji wa habari
B. usafirisha wa bidhaa
C. usikilizaji wa habari
D. matumizi ya vyombo kama simu

**42.** Siku za kisogoni ni ________
A. jana B. siku zilizopita
C. siku zijazo D. siku za usoni

**43.** Ipi kati ya hizi sio njia ya mawasiliano?
A. Teleksi B. Barua
C. Simu D. Kambarau

**44.** Neno jingine la mabwanyenye ni
A. wazee B. majambazi
C. mabingwa D. matajiri

**45.** _______ hushughulikia mtumiaji na upokeaji wa barua kwa mujibu wa kifungu.
A. Shirika la usambazaji umeme
B. Shirika la reli
C. Shirika la posta na simu
D. Shirika la huduma za barua

**46.** Shida la kutumia ujumbe kwa kutumia barua nyakati hizo ilikuwa ipi hasa?
A. Barua zilichukua muda mrefu kuandikwa
B. Gharama ya kutuma barua ilikuwa juu
C. Barua zilichukua muda mrefu kumfikia msomaji
D. Barua zilichukua siku moja au mbili hivi kufika

**47.** Ni nini kilichosaidia kuboresha hali ya mawasiliano kulingana na ufahamu?
A. Uvumbuzi wa tarakilishi
B. Uvumbuzi wa teknolojia mpya
C. Mitambo mipya
D. Shirika la posta na simu

**48.** Ni njia ipi inayofaa zaidi ukitaka kuwasiliana na mtu aliye nga'mbo ukitumia tarakilishi?
A. Simu B. Barua meme
C. Barua D. Rununu

**49.** Kulingana na msemaji katika aya ya mwisho, mtu anapotumia **rukono** anaweza kupiga simu au
A. atume arafa B. apige picha
C. atume picha D. atume pesa

**50.** Faida kubwa ya njia za kisasa za mawasiliano iliyotajwa ni kuwa
A. gharama ya mawasiliani imepungua
B. hata watoto wadogo wana simu na tarakilishi
C. ujumbe unawasilishwa jinsi ulivyotumwa
D. ujumbe unapotumwa mtu hupata papo hapo